**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'**

SHULE YA SEKONDARI ENDAGAW,
S. L. P 265,
KATESH-HANANG'
MANYARA,
02/12/2022.

KUMB. NA. ESS/JNG/K1/2023/Vol.1
MZAZI/MLEZI________________________________

**YAH: KUCHAGULIWA MWANAO KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI ENDAGAW KWA MWAKA WA MASOMO 2023.**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao ........................................................................ amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka wa masomo 2023 katika shule tajwa hapo juu. Nachukua nafasi hii kumpongeza kwa kupata nafasi hii.

*Hongera sana na karibu sana!*

Yafuatayo ni maagizo muhimu ambayo unatakiwa kuyatimiza kabla ya mwanao kuripoti hapa shuleni,

1. Iwapo unaikubali nafasi hii tafadhali jaza fumu ya;
   (a) Kukubali nafasi
   (b) Habari za mzazi au mlezi na mwanafunzi na iwekwe saini.
2. Fika hospitali/kituo cha afya cha serikali na mwanao apimwe na fomu ya kupimwa iliyoambatishwa ijazwe kikamilifu.
3. Fomu zote zilizo tajwa hapo juu zikisha kuwa tayari ufike nazo shuleni na kukabidhi uongozi wa shule siku ya kupokelewa au kuripoti shuleni siku ya tarehe 09/01/2023.
4. Mzazi/mlezi atakayemkosesha mwanafunzi kuripoti shuleni kwaajili ya masomo atachukuliwa hatua kali za kisheria kabla nafasi yake hajapewa mwanafunzi mwingine.
5. Nasisitiza kwamba ni muhimu kila mwanafunzi aripoti siku ya tarehe 09/01/2023 ili kupata fursa nzuri ya kuelimishwa na kuelekezwa masuala mbalimbali ya taaluma, **nidhamu, malezi, sheria za shule n.k**

***Unatakiwa kumuripotisha mwanao shuleni tarehe 09/01/2023 saa 1:30 asubuhi mpaka 6:30 mchana bila kukosa. Mwanafunzi aletwe na mzazi/mlezi wake mwenyewe ili kupokea maelekezo yatakayotolewa na uongozi wa shule.***

**Karibu sana**

THE HEADMISTRESS
ENDAGAW SECONDARY SCHOOL
BOX ______ KATESH
HANANG.

........................
**KINYAMAGOHA L.E**

**MKUU WA SHULE**
**0784 311219**

# MAHITAJI YA SHULE

1. MCHANGO WA CHAKULA
   (a) Mahindi debe tatu (3) kwa mwaka au debe moja na nusu (1½) kwa muhula
   (b) Maharage debe moja kwa mwaka au nusu debe ( ½ ) kwa muhula.
   (c) Fedha Tsh. Elfu arabaini na nne (Tsh 44,000/=) kwa mwaka na Elfu ishirini na mbili (Tsh. 22,000/=) kwa muhula. Fedha hizo zinapokelewa na kamati ya chakula ya wazazi.
   (d) Pia wazazi katika kikao chao wameazima kuchangia ***rim paper*** kwa mwaka kwaajili ya mazoezi.

2. SARE ZA SHULE:
   Mzazi/Mlezi ni wajibu kumshonea mwanao sare kwa mujibu wa Waraka Wa Elimu Bure 2016. Sampuli ya sare na kitambaa kama ilivyoambatanishwa kwenye fomu;

   (a) SARE KWA WASICHANA
   i. Sketi mbili rangi ya kijani kibichi, ndefu inayofika kwenye kifundo cha miguu na blauzi nyeupe mbili mikono mifupi na **zitakakuguliwa. Fuata maelekezo.**
   ii. Sweta moja shingo "V" rangi ya kijani kibichi.
   iii. Tai ndefu ya kijani kibichi.
   iv. Soksi ndefu nyeupe
   v. Viatu vyeusi vyenye kamba na kisigino kifupi
   vi. Saa ya mkononi

   (b) WAVULANA:
   i. Suruali pana zenye (turn up) mbili za kijani kibichi na shati mbili nyeupe mikono mifupi.
   ii. Sweta moja rangi ya kijani kibichi shingo "V"
   iii. Tai ndefu ya kijani kibichi.
   iv. Soksi rangi ya kaki
   v. Viatu vyeusi vyenye kamba na kisigino kifupi
   vi. Saa ya mkononi.

   (c) SARE ZINGINE KWA WOTE
   i. Tisheti ya shule itapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 12,000/=
   ii. Nguo za michezo (track suit) rangi ya "kijani" na zitakaguliwa.

3. MAHITAJI YA KITAALUMA
   i. Daftari 10 (kubwa za kaunta) Quire 2 au Quire 3 na begi zuri na kubwa la kubebea madaftari na si vinginevyo.
   ii. Kalamu za wino mweusi au bluu, penseli, rula, kifutio, mkebe wa hisabati ulio kamilika (mathematical sets)
   iii. Kamusi ya kiingereza moja (English Dictionary)

4. (a) MAHITAJI YA VIFAA VYA USAFI
   i. Fagio mmoja, ndoo ndogo kwa kila mwanafunzi
   ii. Wavulana waje na fykeo na wasichana waje na (mopa)/mopper.

   (b) VYOMBO VYA CHAKULA

Vyombo vya chakula vya aluminium (visiwe vya plastiki), sahani, bakuli, kijiko na kikombe.

"HAIRUHUSIWI KUCHANGIAA CHOMBO WAKATI WA KULA"

MUHIMU: Ikumbuke kuwa siku ya kufungua shule mwanafunzi atalazimika aje na mahitaji yote yaliyoorodheshwa hapo juu, na zoezi la ukaguzi litafanyika kikamilifu. Kuhakikisha mahitaji hayo.

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kw mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978, na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwkaa 1995. pia inazingatia miongozo inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi stadi yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakwa kuzingatia mambo yam sing yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na kupewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni;

(i). Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengne, na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(ii). Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(iii). Kushiriki kwa makini katika shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(iv). Kushiriki na kwa makini a jioni saa 9:00 jioni hadi 11:00 jioni.
(v). Kuwahi katika kila shughuli za shule na utakazopewa.
(vi). Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo .
(vii). Kutunza usafi wa mwili wako,mavazi yako na mazingira ya shule.
(viii). Kuvaa sare kamili ya shule wakati wote uwapo shuleni na katika shughuli zozote utakapotakiwa.
(ix). Kuzingatua ratiba wakati wote na;
(x). Kutunza mali za umma.

**SHERIA,KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE ENDAGAW SEKONDARI**

| NIDHAMU | | |
|---|---|---|
| | KANUNI,SHERIA, NA UTARATIBU | ADHABU INAYOWEZA KUCHUKULIWA |
| 1. | Mwanafunzi anapaswa kuwa na heshima kwa viongozi wa shule,wanafunzi wenzake na jamii kwa ujumla;kushirikiana na wenzake na kuwa mvumilivu.Anapaswa kutii maagizo halali yanayotolewa na walimu pamoja nia viongozi wengine. | Ushauri, onyo **na adhabu kwa kuzingatia sheria na taratibu.** |
| 2. | **Mwanafuni anapaswa utunza na kulinda mali za shule, umma na binafsi** | **Ushauri,onyo,adhabu kwa kuzingatia sheria na taratibu,kulipa gharama za uharibifu.** |
| 3. | **Mwanafunzi anapaswa kushiriki kazi za darasani na kujisomea bila kupiga kelele hata kama mwalimu hayupo.Ikibidi kutoa nje ni lazima kuomba ruhusa kwa mwalimu au kiongozi wa darasa** | Ushauri, onyo **na adhabu kwa kuzingatia sheria na taratibu** |
| 4. | **Mwanafunzi kutembelea nyumba za walimu au watumishi wengine wa shule anapaswa kuwa na sababu maalum** | Ushauri, onyo **na adhabu kwa kuzingatia sheria na taratibu, Kusimamishwa au kufukuzwa shule.** |
| 5. | **Mwanafunzi anapaswa kuheshimu Bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa,Wimbo wa Taifa na Pesa za Taifa wakati wote** | Ushauri, onyo na adhabu kwa kuzingatia sheria na taratibu, Kusimamishwa au kufukuzwa shule |

A. HESHIMA

i. Wanafunzi wawe na heshima kwa walimu, wafanyakazi wote wa shule, wao kwa wao na mtu mwingine yeyote anayewazidi umri.

ii. Wanafunzi hawaruhusiwi kutumia lugha wakati wowote kati yao mwenyewe, kwa walimu wao na kwa watu wengine. **Lugha ya mawasiliano shuleni ni kiingereza tu.**

iii. Wanafunzi wote ni lazima washirikiane na kusaidiana na waheshimu na kuthamini kazi za aina zote.

iv. Wanafunzi wote waharuhusiwi kufanya mambo yafutayo:-

   a. Kuvuta sigara, bangi na kutumia madawa ya kulevya
   b. Kunywa pombe
   c. Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima
   d. Kugombana.

v. Wanafunzi wanatakiwa kuikitia mara moja na kukimbia wanakoitwa

vi. Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu bendera ya serikali, picha za viongozi serikali, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.

vii. Wanafunzi waheshimu ukumbi wa mikutano, ofisi za shule, kutunza na kuthamini mali yao binafsi na mali ya umma.

viii. Wanafunzi wawe mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote walipo.

ix. Wanafunzi wawe kimya wakati wote wakiwa darasani wasitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko.

x. Wanafunzi wanyoshe mkono juu na wasimame wanapoulizwa na kujibu maswali

xi. Wanafunzi kati ya wavulana na wasichana uwe wa kimasomo

B. MUHIMU:

i. Ni lazima wanafunzi wote wahudhurie vipindi vya masomo ndani na nje ya darasa

ii. Wanafunzi wote ni lazima wahudhurie kazi zote za mikono

iii. Wanafunzi wote ni lazima wahudhurie mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha Bendera ya Taifa n.k

iv. Kwa kuzingatia sheria ndogo ya mahudhurio ya lazima katika shule za sekondari Wilaya Hanang' mwanafunzi atakayekosa/acha shule BILA SABABU ZA MSINGI pamoja na MZAZI/MLEZI atakayesababisha mwanafunzi kuacha shule/masomo atachukuliwa hatua za KISHERIA KWA KUZINGATIA SHERIA NDOGO HIYO.

C. KUWAHI

i. Wanafunzi wote ni lazima wawahi shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku, kama vile vipindi vya darasani na nje ya darasa, wakati wa zamu, kurudi shuleni baada ya likizo, n.k

ii. Wanafunzi ni lazima kuwahi haraka wanaposikia wito wa dharura.

D. SARE ZA SHULE

Ni lazima wanafunzi wote wavae sare za shule wakati wa:-

a. Masomo ya darasani
b. Wanapotoka nje kwa shughuli za kishule
c. Mhadhara wa shule (Baraza)
d. Wanapokwenda hospitali

e. Maandamano rasmi
f. Wanakuja shuleni na kurudi nyumbani jioni
g. Kofia, viatu vyenye soli ndefu na mapambo yoyote haviruhusiwi kuvaliwa hapa shuleni
h. Usafi wa sare na mavazi yote yaliyoruhusiwa kuvaliwa shuleni lazima uzingatiwe kila wakati.

E. MIPAKA YA SHULE

i. Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ya kibali/ruhusa maalum na warudi kwa saa zilizoruhusiwa/kupangwa.
ii. Wanafunzi hawaruhusiwi kutembea sehemu zifutazo bila ya kibali maalum:-
    a. Nyumba za walimu na wafanya kazi wasio walimu bila ruhusa maalum.
iii. Marufuku wanafunzi kuwepo sehemu zifuatazo:-
    a. Vilabu vya pombe
    b. Majumba ya starehe
    c. Nyumba za kulala wageni

F. USAFI

i. Kila mwanafunzi ni lazima azingatie usafi wa vifaa vyote anavyotumia hapa shuleni, usafi wake binafsi kama vile; mwili, sare za shule, mazingira ya shu;e n.k
ii. Kila mwanafunzi ni lazima awajibike kwa usafi wa mazingira ya shule, ni marufuku kutupa makaratasi ovyo, na pia ni marufuku kupita njia za vichochoro, kila mwanafunzi lazina atunze bustani za maua kwa kila hali. Nk

## G. MAKOSA YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULENI

i. Wizi

ii. Uasherati

iii. Ulevi wa aina yoyote

iv. Makosa ya jinai

v. Kupigana

vi. Kuharibu mali ya umma kwa makusudi au mali binafsi au ya mtu mwingine

vii. Kudharau bendera ya Taifa/Wimbo wa Taifa

viii. Kuolewa/kuoa

ix. Kupata mimba/kusababisha mimba au kuvuruga Amani na usalama wa watu, lugha za matusi.

x. Kutoa mimba

xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza ua kuvuruga Amani na usalama wa watu, lugha za matusi.

xii. Kukataa adhabu kwa makusudi.

## FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YAKE:

| |
|---|
| *Picha Ya Mwanafunzi* |

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI ENDAGAW,
S. L. P 265,
KATESH-HANANG'
MANYARA.

### A. MWANAFUNZI:

Mimi ..........................................................jinsia (me/ke)...............tarehe ya kuzaliwa.................................Mahali ulipozaliwa kijiji/mtaa ............................. Wilaya .................Uraia ......................................dini ...............dhehebu.............................

Je wewe ni yatima? ..............................................

Nimesoma kwa makini barua ya maagizo ya kujiunga na shule yako, pia sheria za shule.

Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninaikubali/ninaikataa nafasi hiyo kwa sababu .............................................................................................................................

.......................................                                   ..............................

Tarehe                                   Sahihi

| |
|---|
| *picha ya mzazi/mlezi* |

### B. MZAZI/MLEZI;

Mimi.............................................................Mzazi/mlezi wa.............................................

Nimesoma maagizo ya kujiunga na sheria zake. Ninakubali/nakataa nafasi hiyo, ninaahidi/siahidi kumtimizia mtoto wangu mahitaji na maagizo yote ya kujiunga na shule katika muda uliopangwa.

Aidha naahidi kushirikiana daima na uongozi wa shule katika kumtunza na kumlea mtoto huyu kwa manufaa yake binafsi, wazazi na Taifa kwa ujumla. Kama unakataa toa sababu..............................

...........................................................................................................................

N.B:

Udanganyifu wowote ambao utasababisha/kulenga kumkosesha mwanafunzi masomo/shule sheria itachukuliwa dhidi yako. Ahsante.

MAWASILIANO YA MZAZI/MLEZI

Jina la baba: ..........................................Kitongoji:..................simu............saini............

Jina la mama: ........................................Kitongoji: .................Simu: ..........saini .........

Jina la mlezi: ..........................................Kitongoji: .................Simu: ..........saini ..........

NB; NAKALA YA FOMU HII YA KUKUBALI NAFASI NA FOMU YA DAKTARI ZILETWE SIKU YA MWANAFUNZI ANAPORIPOTI SHULENI ZIKIWA IMEJAZWA KIKAMILIFU.

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY.**

**ENDAGAW SEKONDARY SCHOOL P.O.BOX 265 KATESH-HANANG' MANYARA**

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

*To be filled by a Government Medical Officer.*

**Students' Full Name** ..........................................................................................................

**Age** ..............................................................................................................................

**Blood count (Red and White)** ...........................................................................................

**Stool Examination**.............................................................................................................

**Urinalysis** ......................................................................................................................

**Syphilis Test** ..................................................................................................................

**T.B Test** ........................................................................................................................

**Eye Test** ........................................................................................................................

**Ears** ...............................................................................................................................

**Chest** .............................................................................................................................

**Spleen** ...........................................................................................................................

**Abdomen** .......................................................................................................................

**Addition information e.g Physical defects or impairment infections chronic or family diseases etc**..............................................................................................................................
......................................................................................................................................
......................................................................................................................................
..........................................

**TO BE COMPLETED BY A GOVERNMENT MEDICAL OFFICER.**

I certify that the above mentioned student is fit to pursue his/her studies at secondary school.

Signature ............................................

Designation ......................................

Station ..............................................

Date ..................................................